SHULE YA SEKONDARI KIMBE
S. L. P 74
KILINDI

11/12/2020

KUMB Na. ………………………………

JINA LA MWANAFUNZI ……………………………………………………

S. L. P ……………………………………..

………………………………

YAH: <u>MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KIMBE WILAYA YA KILINDI MKOA WA TANGA MWAKA 2021</u>

**1.0. UTANGULIZI**

Ninafuraha kukutaarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021. Shule ya sekondari Kimbe ipo umbali wa km 55 mashariki mwa Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi. Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe 11/01/2021. Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 11/01/2021.

**2.0. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

**2.1. Sare za shule**

a) **Sare ya shule ni Rangi ya Zambarau**, ***wavulana – suruali*** *2* (siyo "Modo", shati nyeupe mikono mifupi na ***wasichana sketi*** 2 rinda boksi 6, shati nyeupe mikono mifupi. Wote viatu vyeusi vya kamba (sio raba), soksi pair 2, tai na sweta rangi ya zambarau, ijabu ifanane na sare ya shule.

b) **Sare za michezo. Wasichana** – fulana ya njano pamija na Track suit- Nyeusi ( yenye suruali, T-shirt na sweta yake).

**Wavulana** – fulana ya njano pamoja na Track-suit nyeusi yenye ( suruali, T-shirt na sweta yake). Wote waje na raba na au viatu vya michezo

2.2. **Vifaa vya Darasani**.

Aje na daftari 15 counter book Quire 3 au 4, kalamu za kutosha, mkebe wa hesabu, kamusi ya kiingereza, file 2 na karatasi za majaribiO Rimu 1.

2.3. Hii ni shule ya kutwa, gharama za chakula zitagharimiwa na mzazi mwenyewe pamoja na matibabu. Hivyo basi awe na bima ya afya. Ili mwanao aweze kujifunza vizuri anatakiwa kula shuleni. Utaratibu wa kula unajulikana kwa wazazi wote wa kata hii ya kimbe namna walivyokubaliana.

2.4. **Usafi –** kila mwanafunzi anatakiwa kuwa na vifaa vifuatavyo:- kwanja, jembe, fagio (chelewa), panga pamoja nan doo.

2.5. **Mavazi baada ya muda wa maasomo** – wasichana – Gauni la light-Blue Mshono wa solo- wavulana – shati/suruali light-Blue.

**<u>Malazi:-</u>** wavulana kwa wasichana, kila mwanafunzi anatakiwa kuwa na mazingira bora ya kupumzikia baada ya masomo, awe na shuka 2 light-blue, Godoro 2.5, mto,Tranja ndogo. **<u>Shule haina nafasi ya hostel.</u>** Hivyo basi , mahali pakuishi mtoto ni jukumu lako mzazi.

**3.0 Sheria na kanuni muhimu za shule hii: -**

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanya kazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla wake ni jambo la lazima.
b) Maudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazo pewa.
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani nan je ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
f) Kutunza usafi wa mwili,mavazi na mazingilra ya shule.
g) Kuvaa sale ya shule wakati wote unapotakiwa.
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
i) Kutunza mali za umma.

**3.2. Mamkosa ya fuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule:-**

a) Wizi
b) Uasherati na Ushoga
c) Ubakaji
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile bangi, cocane, mirungi, kuberi na kadharika.
e) Kupigana au kupiga
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
g) Kudharau Bendera ya Taifa
h) Kuwa mjamzito au kupata mimba
i) Kuoa au kuolewa
j) Kutoa mimba
k) Kugoma,, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
l) Kukataa adhabua kwa makusudi
m) Kuwa na simu ya mkononi na kutumia simu bila kibali.

**4.0. Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na wanafunzi**

a) Medical examination form ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya sserikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.
b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sharia, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

**5.0. Tafadhari soma kwa makini maelekezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

KARIBU SANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI KIMBE

……………………………………

MKUU WA SHULE
SIMU: **0628343067**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI KIMBE
S.L.P 74 SONGE
KILINDI

# TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI

**SEHEMU A:**

1. Jina (kwa herufi kubwa) ……………………………………………………………………
2. Tarehe ya kuzaliwa ………………………………………………(siku, mwezi, Mwaka)
3. Taifa ……………………… mkoa ……………..Wilaya ……………… kabila ……………
4. Taarifa ya kubaini wanafunzi Yatima.

   Weka alama ya (√) panapo husika
   (i) Baba na mama wote walifariki
   (ii) Baba yupo, na mama alifariki
   (iii) Mama yupo, baba alifariki

5. Jina la Baba/ Mlezi ……………………………………………………………………………
   Anuani ya Baba/ Mlezi …………………………………………………………………………
   Namaba ya simu ya Baba/ Mlezi ……………………………………………………………..
   Anauani ya anakofanyia kazi ……………………………………………………………………
   ……………………………………………………………………………………………………

6. Jina la Mama ……………………………………………………………………………………
   Anuani ya Mama …………………………………………………………………………………
   Namaba ya simu ya Mama ………………………………………………………………………

7. Je, Wazazi wako huishi pamoja au wametengana? Ndiyo/ Hapana ………………………………
8. Je, unaishi na wazazi wako wakati wa likizo? Ndiyo/ hapana. Kama huishi nao eleza unaishi na nani?
   Jina ……………………………………………… Anuani yake ……………………………….
   Una uhusiano gani naye …………………………………………………………………………

9. Jina la Dini unayofuata ……………………………………. Dhehebu ……………………………

10. Taarifa za maaelezo zitumwe ka nani?
    Jina ………………………………………… Anuani yake ……………………………………
    …………………………………………………………………………………………...........

11. Umetoka shule gani ……………………………………………………………………………
    Jina la Mkuu wa shule hiyo ……………………………………………………………………
    Anuani ya shule hiyo ni ……………………………………………………………………..
    Namab ya shuke uliyotoka (center No.) ………………………………………………………
    Namba uliyo fanyia Mtihani (Index No.) ……………………………………………………..

# KIAPO

**SEHEMU B:**

Shule ya sekondari Kimbe
S. L. P 74
Kilindi
……………….

## KUKUBALI SHERIA ZA SHULE

JINALA MWANAFUNZI ……………………………………………………………………………………

TAREHE YA KUZALIWA ………………………………………………………………………………….

NAMAB YA SHULE ALIYOTOKA …………………………………………………………………………..

JINA LA MZAZI/MLEZI ………………………………………………………………………………………..

UHUSIANO (UNDUGU) NA MLEZI (BABA, MJOMBA, KAKA) …………………………………………

KAZI YA MZAZI/ MLEZI

KIAPO CHA UTII: MIMI ………………………………………………………………………………….

Nikiwa mwanafunzi wa shule hii nakubali kuwa, umma wanchi hii ya Tanzania ndiyo ulionipa nafasi hii maalumu ya masomo, ili nimalizapo niweze kuitumikia nchi katika maendeleo yake.

Hivyo basi nianaahidi kwamba, nitajibidihisha hapa shuleni na pia nimalizapo shule. Ilikutimiza shabaha hiyo. Ninakubali na kuhaidi kwa hiari yangu mwenyewe kuwa nitatii sharia za shule na amri zote nitakazopewa na walimu wangu.

Nikiwa na malalamiko au maoni niyaponayo bora nitayafikisha kwa viongozi wa shule kufuaatana na utaratibu uliowekwa bila ya kuogopa chochote.

Tarehe ……………………………………….

Sahihi ………………………………………….